**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME**

**SHULE YA SEKONDARI NYASARICHO**

**Barua pepe:** nyasarichoss@tarimedc.go.tz
Namba ya mkuu wa shule: 0754942559/0617642559
Namba ya Makamu wa shule: 0629788403/0689688403
Namba ya mwalimu wa malezi: 0718886608/0758086097

---

**Mzazi/Mlezi wa ………………………………**
**S.L.P …………………………………………**
**……………………………………………...**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI NYASARICHO HALMASHAURI YA WILAYA TARIME MKOA WA MARA MWAKA ……………..**

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule ya sekondari Nyasaricho mwaka ………. Tahasusi ya ……………

Shule ya sekondari Nyasaricho ipo umbali wa Kilometa 11 kutoka Tarime mjini barabara kuu iendayo Sirari. Shule hii ni ya Bweni kwa wavulana kidato cha Tano na Sita, na kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne. Ukitokea Mwanza unashuka Tarime mjini, ukifika Tarime mjini (stand kuu) kuna magari yaendayo Sirari (nauli tsh 2,000) **AU** panda gari zinazokwenda Nyamwaga (nauli tsh 2,000) kisha shuka **Nyamwigura,** Chukua bodaboda atakufikisha Nyasaricho Sekondari (nauli tshs. 3,000). Aidha ukipita njia ya sirari utashuka kituo kinaitwa **Seng'ensa** chukua bodaboda atakufikisha Nyasaricho sekondari (nauli Tsh. 2,000).

Muhula wa masomo unaanza tarehe **………..** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe iliyotajwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

## A. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A.1 SARE YA SHULE

a) Suruali mbili (02) au zaidi zenye marinda mawili pande zote, mifuko mitatu. Moja nyeusi na nyingine kijivu nyeupe (vitambaa viwe namba MOJA) na lazima zishonwe kwa mishono ya kawaida na iwe 1ap indo (turn up), chini size 16).
b) Tai mbili (02) moja nyeusi na nyingine kijivu nyeupe zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 5000/= kwa atakayehitaji
c) Shati mbili (02) au zaidi nyeupe za mikono mirefu na zenye mfuko mmoja tu.
d) T-shirt moja (1) au zaidi zenye colar zitapatikana hapa shuleni (Tsh 15,000/= kwa T-shirt moja
e) Sweta mbili za kuvaa wakati wa baridi (moja blue na nyingine kijivu). Kila sweta litakua na siku yake ya kuvaliwa.
f) Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi mbili (02) visiwe na kisigino kirefu au muundo wa **"BOOT".**
g) Soksi nyeusi jozi mbili (02) na zisiwe na mistari au madoadoa.

h) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi

i) Trak suit rangi ya bluu bahar i(light blue), Bukta ya bluu bahari (light blue) na Raba kwa ajili ya michezo.

***ANGALIZO: Nguo zote za kiraia haziruhusiwi kabisa kuvaliwa shuleni, hivyo mwanafunzi aje na sare (uniform) za kutosha kwa matumizi yake ya kila siku awapo shuleni. Wakati wote mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa kuvaa sare ya shule tu.***

**A. 2 MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE**

| Na. | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| 4 | Nembo (02) | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Tanbihi:** Fedha hii iwekwe kwenye **A/C NO. 0150730646500 CRDB** Jina la akaunti ni **NYASARICHO SECONDARY SCHOOL (DEVELOPMENT A/C**). Mwanafunzi afike na risiti ya malipo yenye Jina lake kurahisisha kazi kwa uhasibu hasa katika ukataji wa Stakabadhi.

**Gharama za mchango wa uendeshaji, tahadhari, kitambulisho na nembo mwanafunzi asije na pesa taslimu mkononi siku ya kuripoti isipokuwa aziweke kwenye akaunti ya benki ya shule**

**A. 3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**

i. Ream nne (02) size A4 (Double A) ya karatasi kwa mwaka
ii. Jembe 1 lenye mpini
iii. Fyekeo 1
iv. Soft broom 1 na Mopa (squizer) 01
v. Ndoo ya lita 20 (1)
vi. Chelewa 01
vii. Dawa ya choo lita 5 inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 10,000/=
viii. Kila mwanafunzi wa tahasusi za sayansi aje na mikasi 01 wa kukatia maua na wanafunzi wa tahasusi za sanaa na brush fupi za chooni (kila mmoja brashi 01)

**A.4 Mahitaji ambayo mwanafunzi anapaswa kuwa nayo kwa matumizi yake bwenini**

i. Shuka mbili (02) za rangi ya bluu bahari (light blue) aje nazo.
ii. Mto na foronya aje nao.
iii. Ndala/ kandambili aje nazo.
iv. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake (ni lazima aje nalo toka nyumbani).
v. Chandarua aje nacho
vi. Taulo aje nayo.
vii. Ndoo ya kuchotea maji na Dumu la lita 5 la kutunzia maji yake ya kunywa. (aje navyo).
viii. Fedha kidogo za matumizi yake muhimu ya kila siku (aje nayo)
ix. Sahani, bakuli, kijiko na kikombe cha nusu lita aje navyo.
x. Aje na blanketi lake la kujifunika kwa sababu ya baridi (Mashuka ya kimasai, vikoi n.k hayataruhusiwa kabisa, na mwanafunzi akikutwa nayo atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa

ni pamoja na kuteketezwa mashuka hayo).

xi. Aje na godoro futi 3x6

xii. Cheti cha ugonjwa kama anacho.

**A.5 Vifaa vya kutumia darasani (aje navyo).**

i) Kikokotozi (calculator) na Mathematical set kwa masomo ya sayansi na hisabati aje navyo ni lazima kitakaguliwa

ii) Lab coat (mavazi ya maabala) kwa masomo ya sayansi: biology, chemistry na physics

iii) Rula, kalamu na penseli za kutosha

iv) Madaftari 8 aina ya counter book 3 quires

v) Vitabu vya masomo ya Tahasusi (combination) husika.

vi) Dissecting kit kwa wanafunzi wa somo la Biology

vii) Kwa masomo ya Lugha waje na kamusi sanifu ya kiswahili au Dictionary (Oxford Advanced Learner's Dictionary) kwa somo la kiingereza

viii) Pia unashauriwa kununua vitabu kulingana na Tahasusi unayosoma.

**Tanbihi**: Vifaa kama Scientific calculator, dissecting kit, lab coat, Kamusi ya Kiswahili (HGK), Dictionary (HGL), godoro, madaftari, kalamu vinapatikana karibu na eneo la shule kupitia Simu na. 0687068021

**B. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama livyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia Miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu; Sayansi na Teknolojia Nchini chini ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Kuhudhuria katika kila shughuli ndani na nje ya shule pale unapohitajika.

iii. Kuhudhuria bila kukosa kwenye maandalio ya jioni (Night Preparation).

iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuepuka kuwa nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.

v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule

vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

vii. Kufuata ratiba ya shule wakati wote.

viii. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki aina yoyote ya silaha mfano kisu, panga, rungu n.k

ix. Kutunza mali za shule na za umma

x. Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki/kuja na simu shuleni

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kurudi nyumbani isipokuwa kwa kibali maalumu

**B.1 Makosa yakayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule**

(i) Wizi wa mali ya shule na wanafunzi wengine.

(ii) Kujihusisha na ngono, uasherati, ushoga, ulawiti, usagaji na ubakaji.

(iii) Ulevi wa pombe na kujihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya

(iv) Kupiga, kupigana au kuchochea ugomvi.

(v) Kuharibu mali ya umma kwa makusudi na kukataa kulipa fidia ya uharibifu

(vi) Kakataa kupokea adhabu halali na kuonyesha kiburi, dharau na ufedhuri,

(vii) Kumiliki; kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

(viii) Kuoa/kuolewa, kupatikana na ujazito, kutoa mimba au kushawishi kutoa mimba.

(ix) Kushiriki au kushawishi kugoma, kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu

(x) Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa au viongozi wa serikali, vyama vya siasa, Madhehebu ya dini na shule.

(xi) Utoro wa muda mrefu kuanzia siku tisini (90) bila taarifa

(xii) Kushindwa kufanya mazoezi/majaribio /mitihani pamoja na kutohudhuria maandalizi ya usiku (Night Preparation).

(xiii) Kutoa lugha ya matusi kwa walimu; wafanyakazi wasio walimu au viranja wa shule.

(xiv) Kulala nje ya shule; kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xv) Kutumia vifaa vya umeme kama vile Heater; redio; pasi ya umeme bwenini

(xvi) Kutembelea nyumba za walimu/watumishi wa shule bila kibali cha mwalimu husika ambao ni mwalimu wa malezi, matron, patron au makamu mkuu wa shule)

(xvi) Kujipikia/kuingiza vyakula bwenini

(xvii) Kukutwa nje ya shule bila ruhusa na mavazi yasiyoruhusiwa shuleni

(xviii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

(xix) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika au kunyoa mtindo wa kihuni

(xx) Kuvuta sigara.

(xxi) Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule ndani ya eneo la shule na nje ya shule.

(xxii) Kupeleka mgeni bwenini ama sehemu nyingine isiyohusika tofauti na maene yaliyoelekezwa.

(xiii) Kujaribu kutumia mafuta yenye kemikali kali ili kubadili mwonekano halisi wa ngozi yako (Kujikirimu)

**C.VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Hospitali ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali (**Mzazi hakikisha kweli mwanao anapimwa afya**) Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara atakaporipoti shuleni.

ii. Fomu ya Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.


iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

v. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

vi. Aje na cheti cha matokeo kidato cha nne" (**aje na cheti orginal)**

**D. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NYASARICHO**




**PASCHAL DAMIAN ISOBU**
**MKUU WA SHULE**

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA TARIME
SHULE YA SEKONDARI NYASARICHO
FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA TARATIBU ZA SHULE.

## SEHEMU YA I: IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE

Mimi..........................................................................nimezisoma sheria; kanuni na taratibu za shule na kuzielewa vizuri bila ya shaka yoyote. Ninaahidi kuzitii na kutozivunja katika kipindi changu chote cha kusoma kwangu katika shule ya sekondari Nyasaricho. Vilevile, nitajitahidi kusoma kwa bidii na kushiriki shughuli zote za nje kulingana na ratiba ya shule. Endapo nitakwenda kinyume na kiapo cha ahadi yangu, basi uongozi wa shule unichukulie hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kupewa adhabu kali/kusimamishwa masomo na hata kufukuzwa shule.
Dini............................... Dhehebu...................... Tarehe ya kuzaliwa............................
Michezo uipendayo/Hobbies..........................................................................................
Kazi ya mzazi/mlezi.................................................. Kijiji/mtaa anaoishi..........................
Wilaya.................................. Mkoa............................. Simu.........................................
Jina la mwanafunzi................................................................... Saini............Tarehe…………

## SEHEMU YA II: IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI.

Mimi.....................................................................ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi……………………………………………. wa kidato cha ………… mwaka 2025; Ninakiri kuwa nimeyasoma maelekezo ya kujiunga na shule ya sekondari Nyasaricho nikiwa na mwanangu na kuyaelewa vizuri. Ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika kuhakikisha kuwa mwanangu anazingatia taratibu zote hizo wakati wa kipindi cha masomo yake. Pia, nitampatia mahitaji yake yote muhimu ya shule ikiwa ni pamoja na malipo ya michango; mahitaji binafsi na kufuatilia mwenendo wake kitaaluma na nidhamu na niko tayari kupokea maamuzi yoyote yatakotolewa na uongozi wa shule endapo mwanangu atavunja taratibu; kanuni na sheria za shule.
Mwisho, endapo nitashindwa kutimiza jukumu langu la kumlipia mwanangu michango halali ya shule kwa wakati, niko tayari kuwajibishwa ikiwa ni pamoja na kufikishwa katika vyombo vya kisheria kwani kufanya hivyo ni kuzorotesha maendeleo ya mwanangu na mipango ya shule na taifa kwa ujumla.
Jina la mzazi................................................................ Saini...........................Tarehe....................

## SEHEMU YA III: UHUSIANO WA MWANAFUNZI NA NDUGU/JAMAA WENGINE.

Tafadhali jaza majina; namba za simu na kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ndugu/jamaa wa mwanafunzi kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano na uongozi wa shule

| NA | JINA LA NDUGU | UHUSIANO | NA. SIMU | ANAKOISHI | KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**SHULE YA SEKONDARI NYASARICHO**

**FOMU YA KUTHIBITISHA AFYA YA MWANAFUNZI**

**(Ijazwe na Mganga wa Hospitali ya Serikali au Kituo cha Afya cha Serikali tu)**

**Kumb. Na. NYSS/MEDICAL/ F.I** **Tarehe ......../......../2025.**

**Mganga Hospitali / Kituo cha Afya...................................................**

S.L.P............................

.....................................

YAH: **KUPIMWA HALI YA AFYA YA MWANAFUNZI ..........................................................**

Shule ya Sekondari Nyasaricho inakuomba kumpima na kujaza taarifa ya Afya ya mwanafunzi mtajwa hapo juu kabla ya kujiunga na masomo ya sekondari.

i Macho (Vision)...................................................................................................................
ii Kifua kikuu (TB).................................................................................................................
iii Pumu (Asthma)...................................................................................................................
iv Shinikizo la Damu (Blood Pressure) ..........................................................................
v Kisukari (Diabetes)..............................................................................................................
vi Magonjwa ya zinaa (Veneral Diseases) .....................................................................
vii Matatizo ya Usikivu (Hearing).........................................................................................
viii Malaria sugu.........................................................................................................................
ix Ulemavu wa viungo (Physical disability). Taja.......................................................
x Mimba kwa msichana (Pregnancy).................................................................................
xi Matatizo akili (Mental disability) ...................................................................................
xii Matatizo ya moyo (Heart problems) ..............................................................................
xiii Matatizo ya tumbo (Abdomen).....................................................................................
xiv Damu (Blood examination) .............................................................................................
xv Kusumbuliwa na kichwa (Headache)...........................................................................
xvi Kichocho (bilharziasis)......................................................................................................
xiii Maradhi mengine (Kama yapo) .....................................................................................
..........................................................................................................................................................

***Kwa namna yoyote ile***: Kama kuna tatizo la kiafya limegundulika; inashuriwa mwanafuzi atibiwe kabla ya kuja shule. Vilevile kwa ugonjwa wowote sugu au wa kurithi shule ipate taarifa

Nimemfanyia mwanafunzi tajwa hapo juu uchunguzi na kugundua kuwa ni mzima/si mzima kiafya na kiakili wa kujinga na shule ya sekondari

Jina la daktari: ................................................................ Saini ……………………..
Cheo .......................................
Mahali pa kazi ……………….
Tarehe ..............................